

## Mabadiliko katika kuboresha huduma za PASS

Katika kuendelea kuwahudumia wateja wetu na kuboresha huduma zaidi, PASS-Trust imefanya madaliko ya mameneja katika matawi yake ya Kigoma na Mbeya.

Katika mabadiliko hayo, Ndg. Ayoub Mbezi ambaye amekuwa afisa wa maendeleo biashara mkoa wa Arusha, sasa atakua meneja wa tawi la Kigoma. Ndg. Ally Mwajasho aliyekuwa kaimu meneja wa mahusiano makao makuu PASS Dar salaam, sasa atakua meneja wa PASS tawi la Mbeya.



**Ayoub Mbezi- Kaimu Meneja wa Kigoma**



**Ally Mwajasho- Meneja Mbeya**



**Leah Mwakangata- Meneja wa Maendeleo biashara**

Akitangaza mabadiliko hayo, mkurugenzi mkuu wa PASS Nicomed Bohay amesema mabadiliko haya ambayo tayari yametekelezwa yanalenga kuboresha

huduma za PASS na kuwapa wafanyakazi fursa ya kufanya kazi katika maeneo mbali mbali nchini.

“Mabadiliko haya yananiua kuongeza ufanisi katika kufanikisha shughuli zetu vile vile kuboresha huduma zetu” Asema Mkurugenzi Bohay

Meneja mpya wa tawi la Kigoma Ndg. Ayubu Mbezi amesema, “nimepokea kwa furaha uteuzi huu na nitafanya kazi kwa bidi ili kuhakikisha PASS inatekeleza malengo yake”

“Nashukuru sana usimamizi wa PASS kwa kuwa na imani na kazi yangu. Nawahakikishia PASS kwamba nitajitahidi kufanikisha shughuli zetu katika tawi la Kigoma na kuboresha mahusiano baina ya wafanyakazi na Wadau washirika wa PASS” Asema Ayoubu.

Naye Meneja wa tawi la Mbeya Ally Mwajasho amesema kwamba “Nimepokea uteuzi huu kwa furaha na nitaendelea kuitumikia PASS kwa hali na mali ili kuboresha maisha ya walengwa wake hali kadhalika kutekeleza malengo yetu PASS ”.

“Kwa kunichagua nirudi tena Mbeya,ni dhihirisho kwamba menejimenti ya PASS ina imani na kazi yangu , hivyo basi natoa shukrani kwa kunirudisha tawi la Mbeya na ninaahidi kujituma ili kuinua tawi liweze kufikia malengo na pia kuyafikia matawi mengine.”alisema Ally.

Hii sio mara ya kwanza kwa Mwajasho kufanya kazi tawi la Mbeya kama Meneja. Awali alikuwa katika tawi hilo na aliamishwa makao makuu katika juhudi za kutekeleza majukumu ya PASS kama kaimu meneja mahusiano.

Wakati huo huo, Bi. Leah Mwakangáta amejiumba na familia ya PASS kama Meneja wa maendeleo biashara. Vile vile Diwani A. Diwani pia amechukua nafasi ya Ayoub kama afisa wa maendeleo biasahara katika tawi la Arusha.